*Mulika, Na. 43 (1), 136-154*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uhakiki wa Kimwingilianomatini katika Fasihi ya Watoto: Mambo ya Msingi ya Kuzingatia

*Rose Jackson Mbijima*[1]
Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.8

**Ikisiri**

Kazi za fasihi ya watoto kama zilivyo kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili zina mwingiliano wa matini wa kiwango cha juu. Hii ina maana kwamba, Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva, ambayo hutumika kuhakiki kazi za fasihi ya watu wazima, hutumika pia kuhakiki kazi za fasihi ya watoto. Kuna mambo ya msingi kadhaa ambayo mtumiaji wa nadharia hii anapaswa kuyazingatia. Hivyo, makala haya yanalenga kubaini mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini. Ili kufikia lengo hili, makala yanaielezea nadharia husika ambapo mawazo yake makuu yanabainishwa na ubora wake kufafanuliwa. Kisha, kazi teule za fasihi ya watoto zinahakikiwa kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini. Kazi za fasihi za watoto zilizohusishwa katika makala haya ni Sababu mimi ni Mwanamke, Kilio Chetu, Ngome ya Mianzi na Marimba ya Majaliwa. Mwisho, makala yanabainisha mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia nadharia hii. Matokeo yanaonesha kuwa mhakiki anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo; kwanza, Nadharia ya Mwingilianomatini ina mawanda mapana. Pili, kiwango cha maarifa aliyonayo mhakiki kuhusu matini chanzo kinaweza kuathiri ufanisi wa uhakiki wa kazi ya fasihi. Tatu, Nadharia ya Mwingilianomatini ina njia bainifu anuai. Nne, Nadharia ya Mwingilianomatini kuhusisha matini zisizo za kifasihi.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanajadili kuhusu Nadharia ya Mwingilianomatini katika kazi za fasihi ya watoto. Kinachoangaziwa kwa umahususi ni mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kutumia nadharia hii katika kuhakiki kazi za fasihi ya watoto. Kwa hiyo, makala yanaielezea nadharia tajwa ambapo misingi na ubora wake inabainishwa. Kisha, makala yamehakiki vitabu teule vinne vya fasihi ya watoto kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini. Vitabu hivyo teule vilivyohusishwa katika makala haya ni: *Sababu Mimi ni Mwanamke* (1999) kilichoandikwa na Ebraju, *Ngome ya Mianzi* (2006) kilichoandikwa na Mulokozi, *Marimba ya Majaliwa* (2008), kilichoandikwa na Edwin Semzaba na *Kilio Chetu* (2008) kilichoandikwa na Medical Aid Foundation. Baada ya uhakiki wa kazi teule, makala yamejadili

[1] **Baruapepe:** rosembijima2019@gmail.com

mambo ya msingi ya kuzingatia katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini, mwisho tumeweka hitimisho la makala.

Pia, katika sehemu hii ya utangulizi tumeeleza dhana ya mtoto. Dhana hii ni pana na ina utata kwa kiasi fulani kutegemeana na muktadha na mwega wa mtoa maana hiyo. Lyimo (2014) anasema kuwa neno mtoto linaweza kufasiliwa kwa kutumia vigezo mbalimbali vya kijamii, kiimani, kiumri na kibaolojia, Kwa mfano, waumini wa dini mbalimbali wanachukuliwa kuwa ni watoto wa Mungu bila kujali umri wao. Kwa wazazi watoto wao wanabaki kuwa watoto hata kama wana umri mkubwa (Bakize, 2014). TUKI (1981) wanafasili dhana ya mtoto kuwa ni mwanadamu au mnyama ambaye hajakomaa au ni jina analoitwa kiumbe ambaye amezaliwa na wazazi wawili. Ndalu na wenzake (2014) wanasema kuwa mtoto ni kiumbe kizaliwacho hususani na mtu. Wafula (2010) anasaidia kuielewa dhana ya mtoto kwa kugawanya watu katika makundi makubwa manne. Anadai kwamba rika la utoto ni miaka 0-17, rika la ujana ni miaka 18-34, rika la wazazi au utu uzima ni miaka 35-52 na miaka 53 na kuendelea ni rika la wazee. Kwa hiyo, kwa mgawanyo huu mtoto ni yule mwenye umri wa miaka chini ya 18. Hivyo, katika makala haya mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18.

### 1.1 Maana na Sifa za Fasihi ya Watoto

Bakize (2014) akimnukuu Wamitila (2010) kwa kuzingatia kigezo cha umri anasema fasihi ya watoto ni ile inayowahusu watu walio chini ya umri wa miaka 18, ambayo inaweza kuwa riwaya, hadithi fupi, tamthiliya, ushairi, hadithi au semi. Kwa hiyo, katika makala haya, fasihi ya watoto ni ile ambayo "Hadhira yake ni watoto na msingi wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto" (Bakize, 2014:2). Vitabu vya fasihi ya watoto vinaweza kuwa vimeandikwa na watoto wenyewe au na watu wazima. Mifano ya kazi za fasihi ya watoto mbali na vitabu teule vya makala haya ni kama vile; *Zindera* (2008) riwaya iliyoandikwa na Sabuni, *Moto wa Mianzi* (1996) na *Ngoma ya Mianzi* (1991) riwaya za Mulokozi, *Mtego Kabambe* (2003) riwaya ya Abeid, *Uduni wangu: Ngonjera za Watoto* (2020) diwani ya ngonjera ya Mbijima, *Safari ya Prospa* (1998) riwaya iliyoandikwa na Lema, *Chanzo ni Wewe* (2015) tamthiliya ya Himu, *Utenzi wa Haki za Watoto* (2003) utenzi wa Abbas, *Kimbia Helana Kimbia* (2005) riwaya ya Mnyaka kwa kutaja chache. Mifano ya kazi za fasihi ya watoto tuliyoitaja hapa, inaweza kugawanyika katika sehemu mbili. Kwanza, kuna kazi za fasihi ambazo zinaweza kuwafaa zaidi watoto wenye umri wa chini ya miaka tisa. Kwa upande mwingine, kuna zile ambazo zinaweza kuwafaa zaidi watoto wenye umri wa miaka tisa hadi kumi na nane, hawa huitwa vijalunga, na kazi zao huitwa fasihi ya vijalunga.

Sifa bainifu za fasihi ya watoto ni pamoja na msuko usiochangamani sana, kuchapwa kwa maandishi makubwa, kuwa na dhamira zinazowahusu watoto, matumizi ya fantansia, kutumia lugha nyepesi, kuwa fupi, kutumia motifu ya safari, wahusika wake ni watoto na kadhalika (Lyimo, 2014; Ngugi na wenzake (2019).

Hata hivyo, baadhi ya sifa za fasihi ya watoto zilizobainishwa zinafanana na sifa za fasihi kwa jumla. Kwa mfano, matumizi ya fantansia na motifu, hayajitokezi tu kwenye fasihi ya watoto, bali hujitokeza hata katika kazi nyingine za fasihi kwa jumla. Jambo jingine la kuligusia kuhusu sifa hizi ni suala la sifa zilizopendekezwa kutokujitokeza kwenye kazi zote za fasihi ya watoto na vijalunga. Kwa mfano, Riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*, ambayo ni mojawapo ya kazi ya fasihi ya vijalunga, haisadifu sifa ya kuchapwa kwa maandishi makubwa ambayo ni sifa bainifu ya fasihi ya watoto. Isitoshe, riwaya hii ni ndefu tofauti na inavyopendekezwa kuwa kazi za fasihi ya watoto zinatakiwa kuwa fupi. Hivyo, tunaweza kusema kuwa siyo lazima sifa zijitokeze zote katika kazi moja ya fasihi ya watoto. Hapa, ufafanuzi wa Kahigi (1995) kuhusu mgawanyo wa ngazi za vitabu vya watoto unaweza kuwa wa muhimu. Kahigi (1995) akizungumzia kuhusu Mradi wa Vitabu vya Watoto anasema kwamba Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania unatambua ngazi tatu za vitabu hivyo ambazo ni Ngazi ya I: Awali hadi Darasa la 2, Ngazi ya II: Darasa la 3 na 4 na Ngazi ya III: Darasa la 5, 6 na 7 (Kahigi 1995:21). Hivyo, ujitokezaji wa sifa za fasihi ya watoto unategemea ngazi husika ya kitabu cha fasihi ya watoto.

## 2.0 Nadharia ya Mwingilianomatini

Nadharia ya Mwingilianomatini ilianzia katika nadharia za isimu za karne ya ishirini, hususani katika kazi za semina za mwanaisimu wa Uswisi, Ferdinand de Saussure. Neno mwingilianomatini lilizuka katika kipindi cha mpito katika miaka ya 1960 huko Ufaransa. Wakati huo Umuundo ulikuwa unajadiliwa sana, jambo lililosababisha kuibuka kwa Umuundompya au Umuundoleo (Allen, 2000). Neno mwingilianomatini lilijitokeza kwa mara ya kwanza katika kazi za Julia Kristeva za *Word, Dialogue and Novel* (1966) na baadaye katika *The Bounded Text* (1966-7) (Allen, 2000; Wamitila, 2003).

Mwingilianomatini umewashughulisha wananadharia wa fasihi kwa muda mrefu, kutoka enzi za kale za Wayunani na Wayahudi; bila shaka kuanzia Aristotle alipofikiria kuhusu umuhimu wa muundo wa tanzia zenye msingi wake kwenye *Iliad* (1961) na *Odyssey* (1974) (Bauman, 2004). Nadharia hii iliibukia kwenye nadharia za lugha jamii, hususan nadharia za fasihi na lugha zilizoasisiwa na Mrusi aliyeitwa Mikhail Bakhtin. Inawezekana Julia Kristeva alipata maelezo ya mwanzo ya Nadharia ya Mwingilianomatini kutokana na nadharia za lugha na fasihi za de Saussure na Bakhtin; hivyo, Kristeva ameathiriwa na mawazo ya Mikhail Bakhtin na Ferdinand de Saussure.

Wamitila (2002) anaeleza zaidi kuhusu nadharia za lugha na fasihi kuwa;

> Dhana ya msingi katika uhakiki wa Bakhtin ni ile ya usemezano. Katika maongezi ya kila siku dhana hii huyarejelea mazungumzo kati ya binadamu. Mazungumzo hayawezi kuwako bila ya kuwako kwa lugha. Bakhtin alisema

> kuwa lugha huwa na sifa za kisemezano. Kwa mujibu wake, kanuni ya usemezano ni muhimu sana. Hii ni kanuni ambayo, mbali na kuchochea, hutawala katika uandishi wowote ule. Bakhtin anasisitiza kuwa maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kisemezano (uk. 151-152).

Wamitila (2002) anaendelea kufafanua kuwa;

> Usemezano unasisitiza kuwa maana ya tamko, usemi au matini haiwi moja bali nyingi na mbalimbali. Kwa Bakhtin matini ya kifasihi ni kama uwanja fulani. Kwenye uwanja huo kuna mwingiliano wa sauti anuwai au aina mbalimbali za usemi. Mhakiki wa matini anapaswa kuziangalia sauti hizo mbalimbali za usemi kama matokeo ya visababishi tofauti tofauti kama tabaka, kundi la kijamii na jamii ya lugha. Bakhtin anaamini kuwa neno au tamko fulani huweza kuwa na maana mbalimbali katika sehemu na wakati tofauti (uk. 151-152).

Hakuna maana moja inayoweza kutolewa kuhusu mwingilianomatini bali ni "Mazungumzo au mjadala baina ya maandiko kadhaa" (Kristeva, 1980:65). Kwa hiyo, "Kila matini ni mwingiliano wa matini nyingine ambamo matini angalau moja inaweza kusomwa" (Kristeva, 1980:66). Mwingilianomatini ni kitendo au mbinu ya kueleza maana ya matini kwa kutumia uhusiano, mfanano, utofauti na muunganiko wake na matini nyingine. Hii ina maana kwamba waandishi hawaundi matini zao kutokana na akili zao za asili, bali wanazitunga kutoka matini zilizopo kiasi kwamba matini ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi. Hivyo, mwingilianomatini ni nafasi ndani ya matini moja ambamo maneno kadhaa, toka matini nyingine, yanaungana na kutanguana. Kwa hiyo, matini zinapata umbo jipya kutokana na marudio na mabadiliko ya matini nyingine (Alfaro, 1996; Bauman, 2004; Wolfreys, 2004; Ogede, 2011).

Kwa hiyo, mwingilianomatini ni mbinu ya kifasihi inayojenga uhusiano baina ya matini na kuleta uelewa unaohusiana katika kazi tofauti. Uhusiano huo unawezesha matini kuwa na tabaka nyingi na kina kirefu kutegemeana na uelewa na ufahamu wa awali wa msomaji wa kazi ya fasihi. Kwa jumla, Nadharia ya Mwingilianomatini inapinga wazo la matini kujitenga, kujitegemea na kujitawala; inasisitiza kwamba matini haiwezi kusimama kama yenyewe bali kwa kuihusisha na nyingine (Alfaro, 1996; Allen, 2000). Tuhitimishe sehemu hii kwa kusema kwamba, kazi ya fasihi si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la mahusiano ya kazi hiyo ya fasihi na kazi nyingine za fasihi na zisizo za fasihi zilizotangulia. Kwamba, mwingilianomatini ni mkakati unaotumiwa na waandishi wa riwaya, ushairi, tamthiliya na hata kazi zisizo za kifasihi**.** Njia bainifu za mwingilianomatini ni unukuzi au kudondoa, tafsiri, udokezo, mwigo wa kubeza na kazi ya sanaa iliyoigwa (Hebel, 1989; Ivanic, 1998; Wamitila, 2003). Kazi za fasihi ya watoto haziwezi kujitenga, nazo zina mwingilianomatini.

Msingi wa nadharia hii ni kwamba wanamwingilianomatini wanaitazama matini kama mahali pa elimumwendo ambapo michakato na matendo ya kiuhusiano ndio kiini cha tathmini badala ya maumbo na mazao ya kielimu mituamo (Irwin, 2004). Kwa kawaida matini hubeba maana fulani. Wasomaji hupata maana ya matini husika wanapoisoma matini hiyo. Kazi za fasihi zinaundwa na mifumo, mila na tamaduni za kazi za fasihi zilizotangulia. Mifumo, mila na tamaduni ni muhimu katika kupata maana ya matini husika. Matini yoyote ikiwa ni ya kifasihi au si ya kifasihi haina maana inayojitegemea isipokuwa ni mwingilianomatini. Kitendo cha kusoma matini kinatuunganisha katika mtandao wa uhusiano matini. Kwa hivyo, kusoma kunakuwa kitendo cha kuhusisha matini nyingi. Maana ya matini inakuwa kitu ambacho kinapatikana katika matini husika na matini nyingine zote zilizorejelewa na zinazohusiana nayo, yaani mwingilianomatini (Clayton na Rothstein, 1991; Allen, 2000).

Naye Wamitila, (2008) anaona kwamba msingi wa Nadharia ya Mwingilianomatini ambao ni fasihi kutokana na fasihi yenyewe, kwa kiasi fulani unaakisi mawazo ya Plato kuhusu mwigo kama msingi wa matendo ya binadamu. Anatoa mfano kuwa mtunzi wa riwaya hawezi kuandika riwaya bila kuwa na picha na taswira ya riwaya iliyotangulia. Kwa hiyo, msingi mkuu wa nadharia hii ni fasihi kutokana na fasihi yenyewe yaani fasihi inaweza kupatikana kwa kuwa pamekuwapo fasihi ulimwenguni (Wamitila, 2008).

Pia, ni muhimu kufafanua sifa za matini yenye mwingiliano wa matini kwamba ina tabia ya kuwa na sifa zinazoipita mipaka yake, kwa sababu vijenzi vyake vinamaanisha vijenzi vya matini nyingi nyingine. Kwa hiyo, ina muunganiko wa pande mbili; matini-ndani ambayo inahakikisha ukamilifu wa ndani wa matini na matini-nje ambayo inahakikisha uhusiano wa kimuundo baina yake na matini nyingine. Mshikamano huu wa namna mbili unafanya matini zilizoingiliana kuwa na utajiri mkubwa wa maana na kuwa changamani. Pia, zinaipa matini sifa ya kuwa na ugumu wa kueleweka kwa wasomaji wengi, hasa wachanga (Clayton na Rothstein, 1991).

Wakati mwingine, matini huweza kubadilisha kabisa umbo lake la ndani kwa ajili ya kupata umbo la nje. Kujiingiza kwa matini ndani ya matini nyingine kunafanya matini hiyo ibadilishe au iachilie mwanzo wake, sehemu yake ya kati na ya mwisho. Inapoteza utambulisho wake wa awali na kujiingiza katika vijisehemu vingi vingine vya matini nyingine ambazo nazo zinarejelea matini nyingine (Leitch, 1983). Vilevile, kazi za fasihi zenye mwingilianomatini zina sifa ya kuhusiana, kuumbuana na hata kuchangamana.

**3.0 Mwingilianomatini katika Kazi Teule za Fasihi ya Watoto**

Sehemu hii ya makala inashughulika na uhakiki wa kazi teule nne za fasihi ya watoto kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini. Tunachofanya katika sehemu hii ni kuonesha jinsi ambavyo kazi za fasihi ya watoto, ambazo zinachukuliwa kuwa ni matini, zimeingiliana na matini nyingine nyingi. Tukumbuke kwamba kwa mujibu wa nadharia hii hakuna kazi ya fasihi ya watoto ambayo haina mwingilianomatini. Bakize (2014:15) akitaja sifa za fasihi ya watoto anaweka uzito kwenye hoja hii anaposema bayana kuwa "katika kazi za watoto mara nyingi mwingilianomatini haukwepeki."

Katika kubainisha matini zilizoingiliana na matini za fasihi ya watoto, tumezingatia si tu matini za kifasihi bali hata zile zisizo za kifahisi. Matini za kifasihi tunazozizungumzia hapa ni tanzu zote za fasihi simulizi na andishi. Mwingiliano wa matini wa namna hii ndio ambao Mbatiah (2001) anauita mwingilianotanzu na anaifasili kuwa ni mbinu ya utunzi wa kazi ya fasihi ya watoto ambapo tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na andishi huchanganywa ndani ya kazi moja wakati wa utunzi wa kazi hiyo. Mbatiah (2001) anaendelea kusema kuwa mwingilianotanzu katika fasihi ni dhana ambayo imekuwa ikijitokeza sana katika kazi za fasihi kutokana na sababu mbalimbali. Wakati mwingine mwingiliano huu hubainishwa na wataalamu wa fasihi simulizi kama mtindo wa kawaida katika kumbo za fasihi. Mmoja kati ya wataalamu wanaobainisha hilo ni Mulokozi (1989) ambaye anasema kuwa mojawapo ya sifa kuu ya fasihi simulizi ni vipera vyake kuingiliana katika utendaji. Hivyo, si ajabu kukuta jina la ngano ni methali, kwa mfano; ngano ya Mkataa Pema, Umdhaniaye Ndiye, Asiyesikia la Mkuu au Usimdharau Usiyemjua (Mbijima, 2020). Hapa kuna mwingiliano wa utanzu wa ngano na methali.

Ingawa ufafanuzi wa Mbatiah kuhusu mwingilianotanzu ni wa muhimu katika makala haya, una dosari. Mbatiah anachanganya dhana mbili: mwingilianotanzu na mwingilianomatini. Anafafafanua kwamba mwingilianotanzu au mwingilianomatini ni istilahi ya kiuumbaji inayomaanisha kuwa matini ya kifasihi siyo thabiti wala kamilifu. Anasema, kifani na kimaudhui zinaingiliana na matini zilizotangulia za kifasihi (Mbatiah, 2001). Kwa hiyo, kwa mtazamo wa Mbatiah (2001) mwingilianotanzu na mwingilianomatini ni dhana zenye maana sawa, jambo ambalo si sahihi. Hata hivyo, pamoja na dosari hiyo, Mbatiah anatukumbusha jambo la msingi anapodokeza kwamba matini huingiliana kimaudhui na kifani; kwa hiyo, katika makala haya tunazingatia mwingiliano wa kimaudhui na wa kifani.

Kwa upande mwingine, matini zisizo za kifasihi ni kama vile matini za kisayansi, kijiografia, kihistoria kiutamaduni kwa kutaja chache. Tukumbuke kwamba kazi za fasihi zinaundwa na mifumo, mila na tamaduni za kazi za fasihi zilizotangulia ambazo ni muhimu katika kupata maana ya matini husika. Kwa hivyo, kusoma kunakuwa kitendo cha kuhusisha matini nyingi. Maana ya matini inakuwa kitu

ambacho kinapatikana katika matini husika na matini nyingine zote zilizorejelewa na zinazohusiana nayo, yaani mwingilianomatini (Clayton na Rothstein, 1991; Allen, 2000). Tunachokisisitiza hapa ni kwamba mwingilianomatini unahusisha pia matini zisizo za kifasihi ambazo zimo katika kazi ya kifasihi. Sehemu inayofuata inahusu uhakiki wa kimwingilianomatini wa kazi teule za fasihi ya watoto.

### 3.1 Mwingilianomatini katika *Sababu Mimi ni Mwanamke*

*Sababu Mimi ni Mwanamke* (1999) ni riwaya ya watoto iliyoandikwa na Ebraju. Mhusika mkuu wa riwaya hii ni mtoto kama anavyodhihirisha mwandishi wa riwaya "umri wangu sasa ni miaka 13. Ninaishi na baba yangu, mama yangu na ndugu zangu wa kiume wawili" (uk. 5). Maudhui ya riwaya hii ni madhara ya tohara kama inavyoeleza mwandishi:

> Tunataka kukusafisha! Uwe mtoto mzuri kama wenzako. Mumeo aweze kukupenda na kukuthamini. Hatuwezi kukuacha na mdudu ndani ya mwili wako… maradhi matupu! Uchafu mtupu! tuangalie sisi wazee wako. Sote tuko safi. Tulisafishwa na wazee wetu. Sasa angalia tunavyopendwa na waume zetu ole wao wasiotahiriwa! (kur. 26-28).

Katika kazi hii ya fasihi ya watoto kuna mwingiliano wa matini wa kiwango cha juu. Kwanza, kuna mwingiliano wa kifani ambapo riwaya imeandikwa kwa kutumia muundo wa barua. Mwanzo wa riwaya hii unathibitisha hilo, mwandishi anaanza riwaya kwa kuandika "Mwenzangu mpendwa" (uk. 1). Huu ni mwanzo ya kibarua. Pia, katika kurasa za 3, 8, 9 na 24, mwandishi anataja wazi kuwa kinachoandikwa ni barua anaposema "Najaribu kuandika barua hii ili kuueleza ulimwengu. Ni matumaini yangu kuwa barua yangu hii ya kwanza utaipata" (kur. 3-4).

Pia, kuna mwingiliano wa wimbo na riwaya. Wimbo unajitokeza katika ukurasa wa 28, 29 na 31. "Mama aliyenibeba alitoka uwanjani, wengine wakafuatia nyuma yake huku wakicheza na kuimba, Mama nyamule hapo, nyamule nifye" wengine waliitikia "nyamule hafe, nyamule hafe" (uk. 31).

Mbali na wimbo, pia katika riwaya hii kuna matini shairi lenye beti 4. Shairi lipo sehemu ya jalada kwa ndani. Linazungumza kuhusu uonevu wa kijinsia. Huu ni mwingiliano wa matini mbili, shairi na riwaya. Hapa tunaona kuwa, mwandishi ametumia mwingilianomatini kama mbinu ya kifasihi kujenga uhusiano baina ya matini hizi mbili na kuleta uelewa unaohusiana katika kazi tofauti yaani riwaya na shairi. Kwa hiyo, kuwepo kwa matini shairi ndani ya matini riwaya kunashadidia madai ya wataalamu wa fasihi kuwa, Nadharia ya Mwingilianomatini inapinga wazo la matini kujitenga, kujitegemea na kujitawala; inasisitiza kwamba matini haiwezi kusimama kama yenyewe bali kwa kuihusisha na nyingine (Alfaro, 1996; Allen, 2000).

Vilevile, kuna mwingiliano mkubwa wa matini andishi na matini simulizi. Kwa kawaida kazi za fasihi andishi huandikwa wakati zile za fasihi simulizi husimuliwa. Kinachoonekana katika riwaya hii ni usimulizi wa kifasihi simulizi. Mwandishi kwa kutumia mhusika wake mkuu anabainisha usimulizi huo. Kwa mfano, katika ukurasa wa 5 anasema "Huu ni mwanzo wa mfululizo wa mikasa mingi ambayo nitakusimulia" (uk. 5). Pia, katika ukurasa wa 10 ametumia mtindo wa fasihi simulizi anasema "Naanza habari zangu kwa kukueleza msiba mkubwa ulionipata. Ilikuwa mwaka jana mwezi wa tano. Siku ilikuwa Jumatatu, mchana" (uk. 10). Vilevile, usimulizi unajitokeza katika ukurasa wa 25 ambapo anasema "ilikuwa alfajiri ya siku moja Jumamosi" (uk. 25). Usimulizi wa namna hii tunaufananisha na ule wa fasihi simulizi. Kwa hiyo, mwandishi ametumia usimulizi wa kifasihi simulizi kama mbinu mojawapo ya kifani ya kuunda riwaya yake. Ingawa usimulizi wenyewe unadokezwa tu bila kuelezwa kwa undani, hata hivyo, tunapendekeza kuwa mtindo huu wa usimulizi ni mwingilianomatini kwa kuwa mojawapo ya njia bainifu za mwingilianomatini ni udokezo. Aidha, mwingiliano huu wa kifani unamaanisha kuwa kiuumbaji matini ya kifasihi siyo thabiti wala kamilifu, kifani na kimaudhui zinaingiliana na matini zilizotangulia za kifasihi (Mbatiah, 2001).

Kwa upande mwingine, kurasa za 24, 25, 27 na 28 zinadhihirisha kuwa jamii inayoelezwa katika riwaya hii ina mila na tamaduni ambazo zinarithishwa kizazi na kizazi. "Kuachishwa shule ilikuwa ndiyo hatua ya kwanza tu. Ilikuwa hatua ya maandalizi. Nilikuwa ninatayarishwa kwa ajili ya jambo jingine la muhimu zaidi kwa mila zetu" (uk. 24). Jambo hilo la muhimu lilijumuisha karibu jamii nzima maana tunaelezwa na mwandishi kuwa bibi wawili wa mhusika mkuu, ambao walikuwa washauri, shangazi yake ambaye alikuwa msimamizi mkuu wa shughuli, marafiki wa mama yake, watani na majirani wote walikuwa wameshafika kutoa msaada wowote uliohitajika. Hawa wote walikuwepo kuhakikisha kuwa mila na tamaduni zinadumishwa na kurithishwa kama anavyobainisha mwandishi "tuangalie sisi wazee wako. Sote tupo safi. Tulisafishwana wazee watu" (uk. 28). Wataalamu mbalimbali wanapendekeza kuwa kazi za fasihi zinaundwa na mifumo, mila na tamaduni za kazi za fasihi zilizotangulia. Mifumo, mila na tamaduni ni muhimu katika kupata maana ya matini husika (Clayton na Rothstein, 1991; Allen, 2000). Hivyo, maana ya riwaya hii ambayo tumesema awali kuwa maudhui yake yanahusu mila na tamaduni za jamii itapatikana kama msomaji wa kazi hii ataelewa mifumo, mila na tamaduni za jamii husika.

### 3.2 Mwingilianomatini katika *Ngome ya Mianzi*

*Ngome ya Mianzi* ni riwaya ya watoto iliyoandikwa na Mulokozi na kuchapishwa mwaka 2006. Riwaya inahusu hadithi ya vita kati ya Wahehe na Wadachi ambavyo vilipiganwa mwaka 1885-1900 huko Lugalo Iringa katika nchi ya Tanzania. Katika riwaya hii kama kazi nyingine za watoto zilivyo, kuna mwingiliano wa matini mbalimbali za kifasihi na zisizo za kifasihi. Matini zisizo za kifasihi zilizomo katika

riwaya hii ni kama vile matini ya kijiografia na kihistoria. Sehemu inayofuata tunabainisha matini mbalimbali zilizoingiliana katika riwaya tajwa.

Kwanza, katika riwaya ya *Ngome ya Mianzi* (2006), kuna mwingiliano wa matini wa riwaya na nyimbo. Mwandishi anasema "kabla hatujafika juu ya kilima watu walianza kutushangilia na kutuimbia nyimbo za kutusifu walizozitunga hapohapo. Watu waliimba: *Salamuni mashujaa Wahehe twawatukuza mmetenda ya kufaa mazimwi kuteketeza…"* (kur. 42-43). Katika wimbo huu, mashujaa wanasifiwa kwa kuweza kuyateketeza mazimwi. Kwa kawaida mazimwi ni wahusika wa fasihi simulizi hususani kipera cha ngano (Senkoro 1991; Mulokozi 2017). Matumizi ya wahusika wa kifasihi simulizi yanadokeza mwingiliano wa matini hii ya riwaya na matini ya fasihi simulizi, yaani ngano. Mwingiliano wa matini ya riwaya ya *Ngome ya Mianzi* (2006) na matini ya ngano, unafanya riwaya tajwa kuwa na sifa zinazoipita mipaka ya riwaya, kwa sababu vijenzi vyake vinamaanisha vijenzi vya kifasihi simulizi yaani ngano. Kwa hiyo, riwaya hii inakuwa na muunganiko wa pande mbili yaani matini-ndani ambayo inahakikisha ukamilifu wa ndani wa riwaya na matini-nje ambayo inahakikisha uhusiano wa kimuundo baina yake na fasihi simulizi.

Vilevile, kuna matini ya kihistoria, ambapo riwaya nzima imejengwa juu ya kisa cha kihistoria. Kwa kushadidia hili, mwandishi mwenyewe katika dibaji anaeleza kuwa hii ni riwaya ya kihistoria. Historia inayoelezwa humu ni ya vita vya Lugalo vilivyopiganwa kati ya Wahehe na wavamizi wa Kidachi mwaka 1891. Katika ukurasa wa 23 bibi anamsimulia Mugoha kuhusu mashujaa wa kabila lao anasema, "Tulikaa kwa muda mrefu tukiongea hili na lile. Bibi alinisimulia kidogo habari za mashujaa wa zamani wa kabila letu, kina Muyinga na Munyigumba. Halafu alinieleza habari za Mutwa, Mtemi wetu Mukwava na jinsi alivyopambana na Waarabu wateka watumwa." (uk. 23). Isitoshe, pamoja na matini ya kihistoria kuhusu vita vya Wadachi, kuna *Utenzi wa Wadachi* ambao ni kazi ya fasihi, inayohusu historia ya vita hivyo. Hapa kuna mwingiliano wa matini riwaya na utenzi wa kihistoria, utenzi wa vita vya Wadachi. Kwa hiyo, kitendo cha kusoma riwaya ya *Ngome ya Mianzi* kinatuunganisha katika mtandao wa uhusiano matini kati ya matini ya kihistoria kuhusu vita vya Wadachi na kabila la Wahehe na matini ya kishairi ya *Utenzi wa Vita vya Wadachi*. Hivyo, kusoma kunakuwa kitendo cha kuhusisha matini nyingi. Maana ya matini ya riwaya ya Ngome ya Mianzi inakuwa kitu ambacho kinapatikana katika matini ya riwaya hii na matini nyingine zote zilizorejelewa yaani matini ya kihistoria na matini ya *Utenzi wa Vita vya Wadachi*.

### 3.3 Mwingilianomatini katika Tamthiliya ya *Kilio Chetu*

*Kilio Chetu* (2008) ni tamthiliya ambayo imeandikwa na Medical Aid Foundation, inaeleza kuhusu matatizo ambayo chimbuko lake ni mahusiano ya kimapenzi. Matatizo hayo ni mimba za utotoni pamoja na maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI kwa vijana wadogo na hatimaye vifo vinavyosababishwa na maambukizi

hayo. Hivyo, katika tamthiliya hii wahusika, ambao ni vijalunga, wanapaza sauti yao kwa wazazi, walezi na viongozi ili wawape elimu kuhusu mahusiano ya kijinsia badala ya kunyamaza kimya hali wanaangamia kwa kukosa elimu. Kama zilivyo kazi nyingine za fasihi ya watoto, katika tamthiliya hii kuna mwingiliano wa matini kama ifuatavyo:

Kwanza, kuna mwingilianomatini wa tamthiliya na wimbo. Huu ni mwingilianomatini baina ya matini ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Kwenye ukurasa wa kwanza wa tamthiliya ya *Kilio Chetu*, kiongozi anaanzisha wimbo na watu wanaitikia. Wimbo umeandikwa:

| | |
|---|---|
| *Kiongozi:* | *Twaangamia x 4* |
| *Watu:* | *Tunakwisha tunakwisha* |
| | (*Kilio Chetu*, 2008:1) |

Pia, kuna wimbo mwingine ukurasa wa 39, ambapo waombolezaji wanaimba baada ya Joti kufariki kwa UKIMWI, wimbo ambao una maana ya Joti amevaa sanda.
Mbali na nyimbo, kuna mwingilianomatini wa tamthiliya na ngano ambayo inadhihirishwa na matumizi ya kaida za kifasihi simulizi. Kuna matumizi ya mianzo na miisho ya kifomula simulizi ambayo yanaashiria hadithi za kifasihi simulizi yaani ngano. Fomula hizo ni kama vile:

| | |
|---|---|
| Mtambaji: | Paukwa. |
| Wote: | Pakawaaaaaaa. |
| Mtambaji: | Hapo zamani za kale paliondokea kisiwa kimoja kikubwa sana. Kisiwa kilikuwa na watu wa kila aina. Kulikuwapo matajiri na kulikuwapo masikini. Watu waliishi kwa furaha sana…Niseme nisisema. |
| Wote: | Sema. |
| Mtambaji: | Niendelee nisiendelee. |
| Wote: | Endelea (*Kilio Chetu*, kur. 1, 2, 40). |

Isitoshe, mwisho wa kitabu ukurasa wa 40, mwandishi anahitimisha tamthiliya yake kwa fomula za fasihi simulizi "Na hadithi yangu imeishia hapo." Senkoro (2011) akifafanua kuhusu mianzo na miisho ya kifomula anasema kuwa, "Kuhusu kumalizia hadithi, mara nyingi mtambaji humaliza kwa, "Na hadithi yangu imeishia hapo au hadithi yangu ndiyo hiyo, kama nzuri ipokeeni kama mbaya nirudishieni" (Senkoro, 2011:69). Vilevile, Senkoro (2011) anaweka bayana kuwa mwingilianomatini siyo tu matumizi ya utanzu wa fasihi ndani ya mwingine bali hata ujitokezaji wa sifa za utanzu fulani ndani ya utanzu mwingine. Kwa hiyo, matumizi ya sifa za fasihi simulizi, yaani mianzo na miisho ya kifomu ndani ya tamthiliya, ni mwingilianomatini baina ya matini hizo tajwa. Mwingiliano wa tamthiliya ya *Kilio chetu* na matini za kifasihi simulizi kama nyimbo na ngano, unathibitisha madai ya wataalamu wa fasihi kuwa mwingilinomatini ni

"Mazungumzo au mjadala baina ya matini kadhaa. Kila matini ni mwingiliano wa matini nyingine ambamo matini angalau moja inaweza kusomwa" (Kristeva, 1980:65-66). Kutokana na mwingiliano wa matini hizi, maana ya tamthiliya ya *Kilio chetu* inatakiwa kuelezwa kwa kutumia uhusiano, mfanano, utofauti na muunganiko wake na matini za fasihi simulizi zilizomo ndani yake yaani nyimbo na ngano. Hii ina maana kwamba mwandishi wa tamthiliya tajwa hakuunda tamthiliya yake kutokana na akili zake za asili, bali kutoka matini zilizopo kiasi kwamba *Kilio chetu* ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi.

### 3.4 Mwingilianomatini katika *Marimba ya Majaliwa*

*Marimba ya Majaliwa* (2008) ni mojawapo ya kazi za fasihi ya watoto. Riwaya hii iliandikwa na Edwin Semzaba. Kama ilivyo kwa kazi nyingine za fasihi ya watoto, kuna mwingilianomatini katika riwaya tajwa. Hata hivyo, mwingilianomatini katika riwaya hii ni wa kiwango cha juu kuliko katika kazi nyingi za fasihi ya watoto. Ufafanuzi ufuatao unadhihirisha kauli hii kama ifuatavyo:

Kwanza, kuna mwingilianomatini wa riwaya na nyimbo mbalimbali katika kurasa za 1, 2, 4, 6, 8, 10, 11, 16, 24, 38, 61, 83, 97, 102, 116, 201, 226, 233 na kadhalika, japo tungo nyingi ambazo mwandishi anaziita nyimbo si nyimbo bali mashairi. Kwa mfano, ukurasa wa 16 mwandishi anasema, "Majaliwa akakumbuka wimbo:

> Umewaondoa kedi, makabaila kulamba
> Walitawala kusudi, damu yetu kuilamba
> Pahali si yao jadi, walijifanya miamba
> Simba wa visiwa tamba, Sheikh Karume Abeid
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 16).

Katika nukuu hii tunaona mwingiliano wa riwaya na shairi ambalo mwandishi anasema ni wimbo. Kutokana na wataalamu mbalimbali wa fasihi akiwemo Mulokozi (2017), mfano tulioutoa hapo juu una vigezo vyote vya kuitwa shairi badala ya wimbo. Vigezo hivyo ni pamoja na mishororo, mizani, vina na kitoshelezo ambavyo ni sifa bainifu za shairi la kimapokeo. Hata hivyo, hatutajadili kwa kina suala la uchanganyaji wa wimbo na shairi unaofanywa na mwandishi wa riwaya hii kwa kuwa siyo lengo letu. Aidha, kuna mwingiliano wa matini baina ya riwaya hii na wimbo wa *Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote*, ukurasa wa 24 na 62:

> Tanzania Tanzania
> Ninapokwenda safarini
> Kutazama maajabu
> Biashara nayo makazi
> Sitaweza kusahau mimi
> Mambo mema ya kwetu hakika
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 62).

Pia, kuna mwingiliano wa matini wa riwaya hii na wimbo wa *Malaika* ukurasa wa 38:

> Malaika nakupenda malaika
> Malaika nakupenda malaika
> Nami nifanyeje
> Kijana mwenzio
> Nashindwa na mali sina wee
> Ningekuoa malaika
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 38)

Vilevile, kuna mwingiliano wa matini baina ya riwaya hii na wimbo wa *Sisi tumekwisha kuuwasha mwenge, tumekwisha kuuwasha mwenge* ukurasa wa 61:

> Sisi tumekwisha kuwasha mwenge
> Tumekwisha kuwasha mwengex2
> Na kuuweka juu ya mlima
> Mlima Kilimanjarox2
> Kuwasha mwenge kuwasha mwenge
> Na kuuweka Kilimanjarox2
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 61)

Halikadhalika, kuna wimbo wa *Tazama ramani* ukurasa wa 87.

> Tazama ramani
> Utaona nchi nzuri
> Yenye mito na mabonde
> Mengi ya nafaka
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 87)

Aidha, katika ukurasa wa 184-185 kuna mwingiliano wa riwaya na kitabu cha *Mashairi ya Shaaban Robert*. Mwandishi mwenye anathibitisha hilo anaposema, “Shairi letu ni la Shaaban Robert, linaitwa “Siku ya Kutukuka” kutoka kitabu cha *Mashairi ya Shaaban Robert*” (Semzaba 2008:184). Mwandishi anasema:

> Ilikuwa ni usiku, kabla ya kupambazuka
> Wa kule haoni huku, giza bado kutoweka
> Kabla kulia kuku, na umande umeshuka
> Alipoipata Mkwawa, siku ya kutukuka
> (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 184)

Vilevile, kuna mwingiliano wa riwaya na kitabu cha Mugyabuso Mulokozi cha *Mukwava wa Uhehe* katika ukurasa wa 185-187. Mwandishi mwenye anathibitisha mwingiliano huu anaposema “Shairi letu linatoka katika kitabu cha Mukwava wa Uhehe cha Mugyabuso Mulokozi. Linaitwa Maneno ya mwisho ya Mkwava” (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 185).

Isitoshe, kuna matumizi ya utanzu wa majigambo, ambao mwandishi anauita utambaji wa kusifu ukurasa wa 147. Mbali na hayo, kuna matumizi ya utanzu wa enanga mamboleo ukurasa wa 148.

Mbali na mashairi na nyimbo katika riwaya hii, kuna mwingiliano wa utanzu wa ngonjera ndani ya riwaya, ukurasa wa 66-67, ambapo watambaji wawili wanaulizana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

> MTAMBAJI WA KWANZA
> Wenzangu niambieni, kuna jambo latatiza,
> Kumeingia nchini, ugonjwa wa kushangaza,
> Nauliza hadharani, mnipatie mwangaza,
> Huu ni ugonjwa gani, tafadhali nambieni.
>
> MTAMBAJI WA PILI
> Tulia tunakuambia, mwananchi ujihadhari,
> Ugonjwa umeingia, ni wenye kubwa hatari,
> Hauna cha kukingia, twakupasha hii habari,
> Unaitwa UKIMWI, mwili kuikosa kinga (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 66)

Aidha, kuna mwingiliano wa kimaudhui na kifani baina ya riwaya tajwa na riwaya ya *Wasifu wa Siti binti Saad* ya Shaaban Robert; kwa mfano, wahusika wa riwaya ya *Siti bint Saad* kama Siti binti Saad wametumika ndani ya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*.
Pia, kuna mwingiliano wa matini za kihistoria. Mathalani katika ukurasa wa 14 mna mwendesha baiskeli anamweleza Majaliwa kuhusu soko la watumwa. Anasema;

> "Hapa ni Mkunazini. Hapo zamani wakati wa enzi za utumwa, sehemu hii ilikuwa soko la watumwa. Walipofika hapa kutoka sehemu mbalimbali za bara, watumwa waliuzwa na kusafirishwa kwenda Uarabuni na sehemu nyingine. Utumwa ulipokomeshwa ndipo Edward Steere akajenga hili kanisa" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 14).

Isitoshe, ukurasa wa 16, kuna historia ya mzee Abeid Amani Karume, mwanamapinduzi thabiti na rais wa kwanza wa Zanzibar. Mwandishi anasema;

> "Majaliwa aliachiwa na askari yapata saa kumi na mbili jioni kukiwa bado kweupe. Alitembeatembea mjini, akafika hadi ofisi ya CCM Kisiwandui, akaona kaburi la Abeid Amani Karume, mwanamapinduzi thabiti aliyeongoza wananchi katika mapinduzi yaliyong'oa usultani wa Kiarabu uliofika visiwani humo tangu mwaka 1832" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 16).

Aidha, katika ukurasa wa 41 tunadokezwa historia ya mji wa Pangani Tanga ambapo Bushiri bi Salim aliwahi kupiga kambi karne ya kumi na tisa. Vilevile,

mwandishi anachomeka matini ya kihistoria kuhusu kaburi la Shaaban Robert anaposema;

> "Njiani kuelekea Tanga, Majaliwa aliona minazi mingi na mashamba ya katani. Walipokuwa wakiingia Tanga, Majaliwa alisoma alama ya barabarani ikionesha mshale kuelekea kulia na maneno VIBAMBANI. Hakufahamu umuhimu wa sehemu iliyoelekezwa, hivyo hakutambua kuwa Vibambani kuna kaburi la mwandishi maarufu wa Kiswahili, Shaabani Robert aliyefariki mwaka 1962. Shaaban Robert aliipenda lugha ya Kiswahili na aliilinganisha na titi la mama ambalo haliishi utamu" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 41).

Pia, ukurasa wa 145, bibi anamsimulia Majaliwa historia ya Kaitaba, mtawala wa Kyamtwara Bukoba. Mwandishi anaendelea kueleza kuhusu Mfalme Ruhinda aliyevamia Karangwe miaka ya 1858 ambaye haongelewi sana kwenye historia ya Wazungu. Katika ukurasa wa 104, kuna matumizi ya matini ya kihistoria kuhusu mapango ya Kondoa Irangi mahali ambapo kuna kumbukumbu ya michoro ya watu wa kale. Habari hii inaendelea ukurasa wa 105 ambapo bibi anataja sehemu nyingine za kihistoria Tanzania hususani katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Singida. Pia, kuna matini ya kihistoria kuhusu ajali ya meli ya MV Bukoba ukurasa wa 143, ambapo bibi anamweleza Majaliwa kuwa;

> "Chini yetu kuna masalia ya meli ya M. V. Bukoba. Ngoja nikuguse juu ya macho ili uweze kuiona ilipolala. Bibi alimgusa Majaliwa machoni na mara akaliona gofu la M. V. Bukoba ndani ya maji. Hee ni meli kubwa sana! Tena imeanza kupata kutu. Majaliwa alishangaa" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 143).

Mifano hii inaonesha wazi kuwa katika riwaya tajwa kuna mwingiliano mkubwa wa matini za kihistoria.

Aidha, riwaya hii ina mwingiliano na matini za kijiografia. Kwa mfano; ukurasa wa 38 kuna matini ya kijiografia ambapo zinatajwa aina za nyota na sayari mbalimbali kama vile zuhura, zebaki na kadhalika. Matini nyingine ya kijiografia ipo ukurasa wa 147, ambapo tunadokezwa wilaya zote za mkoa wa Kagera mwandishi anasema "Mkoa wa Kagera, ambao una wilaya, yaani; Ngara, Biharamulo, Muleba, Bukoba, Karangwe na Missenye ulitoa washindani kumi, wawili kutoka katika kila wilaya" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 147).

Isitoshe, kuna matumizi ya mianzo na miisho ya kifomula ya kifasihi simulizi ambayo yanaashiria mwingiliano wa matini andishi yaani riwaya na matini simulizi yaani hadithi, kwa mfano, fomula ya niendelee nisiendelee, paukwa pakawa ukurasa wa 23 na 24. Pia, kuna ngano ya Kibo na Mawenzi, kuna matumizi ya

hadithi ya mvuvi ukurasa wa 167 na hadithi nyingine kama vile ugomvi kati ya bibi na babu yake Majaliwa.

Halikadhalika, kuna mwingiliano wa riwaya na dini za jadi. Kwa mfano, ukurasa wa 143 kuna viumbe wanaotembea tembea kwenye masalia ya meli ya MV Bukoba na bibi anamwambia Majaliwa kuwa hao ni mizimu ambao baada ya meli kuzama na kuwa gofu mizimu ya himaya ya Mugasha, mfalme wa ziwa Viktoria, inakaa.

> "Mugasha ana nguvu sana. Hekalu lake liko visiwa vya Sese. Baadaye tutakapoachana sina budi kupita huko nikatoe heshima zangu. Mugasha ni mungu wa mvua. M. V. Bukoba ilipozama alifanyiwa matambiko huko usukumani. Mugasha ana mke anaitwa Nyakirembe, ni mungu wa kilimo" (*Marimba ya Majaliwa*, uk. 143).

Pia, katika ukurasa wa 144, bibi anamsimulia Majaliwa kuhusu visiwa vitatu, Ukerewe, Ukara na Irugwa. Anamweleza kuhusu jiwe linalocheza kwa uweza wa ajabu wa Mugasha. Uhakiki wa kimwingilianomatini umetuwezesha kubaini kuwa riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ina mwingiliano mkubwa na matini mbalimbali kiasi kwamba riwaya imeweza kubadilisha kabisa umbo lake la ndani kwa ajili ya kupata umbo la nje. Kujiingiza kwa matini za nyimbo, mashairi, ngano, tamthiliya na hata riwaya nyingine, kumefanya riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ibadilike kiasi cha kupoteza utambulisho wake wa awali na kujiingiza katika vijisehemu vingi vingine vya matini zilizomo ndani yake ambazo nazo zinarejelea matini nyingine. Vilevile, kwa kuingiliana na matini mbalimbali ambazo tumezionesha hapo juu, riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* inakuwa na sifa ya kuhusiana, kuumbuana na hata kuchangamana na matini hizo.

Sehemu hii imejikita kujadili jinsi ambavyo kazi teule za fasihi ya watoto zimesheheni matini kadha wa kadha ndani yake. Mjadala mzima umeegemezwa na mawazo ya Nadharia ya Mwingilianomatini. Sehemu inayofuata inajihusisha na mjadala kuhusu mambo ya msingi ya kuzingatia katika uhakiki wa kimwingilianomatini katika kazi za fasihi.

## 4.0 Mambo ya Msingi ya Kuzingatia katika Uhakiki wa Kimwingilianomatini

Baada ya kuhakiki kazi za watoto kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini katika sehemu iliyopita, katika sehemu hii tunajadili mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia nadharia tajwa. Kwa jumla mambo hayo yapo kadhaa kama tunavyoyajadili hapa chini.

### 4.1 Nadharia ya Mwingilianomatini ina Mawanda Mapana

Jambo mojawapo la kuzingatia wakati wa kufanya uhakiki wa kimwingilianomatini ni kufahamu kuwa nadharia hii ina mawanda mapana. Dhana ya mwingilianomatini ni pana na inajumuisha vitu vingi. Pia, mwingilianomatini hauna kikomo, kwani

matini yoyote inaweza kuingiliana na matini nyingine yoyote. Hii ina maana kwamba maana ya matini yoyote haina mwisho na hivyo maana haiwezi kukamilika wala kutabirika. Mfano mzuri ni mwingilianomatini katika riwaya ya *Marimba ya Majaliwa* ya Semzaba, na matini nyingine kama vile nyimbo mbalimbali kama vile *Tanzania Tanzania*, wimbo wa taifa la Tanzania; *Mungu ibariki Tanzania*, kuna wimbo wa *Tazama Ramani*, kuna utajiri wa ngano ndani ya riwaya hii na kadhalika. Isitoshe, kuna matini nyingi zisizo za kifasihi ndani ya riwaya kama tulivyoona katika sehemu iliyopita.

Nayo riwaya ya *Ngome ya Mianzi* kwa mfano, imeundwa kutokana na tukio la kihistoria la vita vya Wadachi na Wahehe lililotokea zamani, inamlazimu msomaji kuwa na uelewa mpana kung'amua mwingiliano katika riwaya hii. Kinachobainika wazi hapa ni kwamba, dhana ya mwingilianomatini ina mawanda mapana. Ili msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi aweze kuelewa na kupata maana ya kazi ya fasihi, iliyokusudiwa inamlazimu kuwa na uelewa mpana wa matini mbalimbali. Vinginevyo, ni vigumu kubaini ujumbe wa kazi husika. Isitoshe, mwingilianomatini ni dhana inayomeza matini zisizo za kifasihi pia, jambo ambalo linaongeza upana wa nadharia hii.

### 4.2 Ufanisi wa Uhakiki wa Kimwingilianomatini Unategemea Kiwango cha Maarifa Alichonacho Mhakiki kuhusu Matini Chanzi

Suala jingine muhimu la kuzingatia ni kwamba ufanisi kwa kutumia nadharia tajwa unategemea kiwango cha maarifa alichonacho mhakiki kuhusu matini chanzi. Tumefafanua awali kwamba Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kwamba kila matini imeingiliana na matini nyingine. Kwa hiyo, kuielewa na kuifurahia matini husika kunategemea kiwango cha maarifa aliyonayo msomaji kuhusu matini chanzi. Ukweli ni kwamba wasomaji wa matini hawana maarifa, historia na tajiriba sawa kwa hivyo hata fasili yao hutofautiana. Hoja ya msingi hapa ni kwamba, kama jinsi nadharia ilivyopana, ndivyo ambavyo mhakiki anatakiwa kujua matini mbalimbali kwa upana huohuo vinginevyo inakuwa vigumu kwa mhakiki kung'amua matini mbalimbali zilizomo ndani ya kazi husika. Kwa hiyo, tunaweza kusema kiwango cha mwingilianomatini kinategemea kiwango cha maarifa aliyonayo mhakiki. Mfano mzuri hapa ni Vita vya Wadachi na Wahehe vya mwaka 1885-1900 ambalo ni tukio la kweli katika historia ya nchi ya Tanzania, lakini kuna kazi ya fasihi inayoitwa *Utenzi wa Vita vya Wadachi*.

Mulokozi katika riwaya ya *Ngome ya Mianzi* amehusisha vita vya Wadachi kama tukio na *Utenzi wa Vita vya Wadachi* kama kazi ya kifasihi. Ili mhakiki au msomaji wa riwaya ya *Ngome ya Mianzi* aweze kubaini kuwa kuna mwingiliano wa matini ya kihistoria na ya kishairi yaani utenzi katika riwaya hiyo, lazima awe na maarifa kuhusu matini chanzi hizo, yaani hiyo vita na huo utenzi. Kwa hiyo, hapa, tukio la vita na Utenzi wa Vita vya Wadachi ni matini chanzi mbili tofauti. Mfano mwingine ni mashairi ya Shabaan Robert ambayo Semzaba ameyatumia katika

riwaya yake ya *Marimba ya Majaliwa* pamoja na riwaya ya Shaabani Robert ya *Siti Binti Saadi*. Ugumu unaojitokeza hapa ni huo ulazima wa mhakiki kuwa na maarifa kuhusu matini chanzi zilizotumika katika matini inayohakikiwa ili kuweza kuubaini huo umwingilianomatini wenyewe.

**4.3 Mwingilianomatini una Njia Bainifu anuai**

Mhakiki wa kimwingilianomatini anapaswa kuzingatia kuwa kuna njia bainifu kadhaa za Nadharia ya Mwingilianomatini ambazo ni unukuzi au kudondoa, tafsiri, udokezo, mwigo wa kubeza na kazi ya sanaa iliyoigwa. Hii ina maana kuwa mara nyingi matini zilizoingiliana hudokezwa tu kwa kifupi jambo linaloweza kutatiza ubainishaji wa matini ndani ya matini nyingine. Aidha, wakati mwingine mwingilianomatini huhusisha ujitokezaji wa sifa za utanzu au matini ndani ya utanzu au matini nyingine. Sifa hizo zinaweza kuwa mianzo na miisho ya hadithi za kifasihi simulizi ndani ya fasihi andishi, majibizano ya kitamthiliya ndani ya riwaya au ushairi na kadhalika, kama tulivyoona kwenye uhakiki. Kwa jinsi hii ni muhimu kuzingatia kuwa matini zilizoingiliana na kazi tajwa ya fasihi hazielezwi kwa undani na kwa mapana. Kama mhakiki hazijui kwa undani matini chanzi itamuwia vigumu kubaini mwingiliano wa matini hizo. Kwa mfano, matumizi ya fomula simulizi ndani ya *Kilio Chetu* yamedokezwa tu, inahitaji maarifa ya mhakiki kubaini kuwa ni sifa za fasihi simulizi kabla hajabaini kuwa ni mwingilianomatini. Mfano mwingine ni mwingiliano wa kifani wa muundo wa barua na riwaya ya *Sababu Mimi ni Mwanamke* ambao unadokezwa tu mwanzoni mwa riwaya tajwa bila kuelezwa kwa undani.

**4.4 Mwingilianomatini katika Kazi za Fasihi Huhusisha Matini Zisizo za Kifasihi**

Aidha, ni muhimu kuzingatia kuwa mwingilianomatini unahusisha pia matini ambazo si za kifasihi ndani ya matini za kifasihi. Matini hizo ni kama vile matini za kijiografia, kihistoria, kidini, kisayansi na kitabibu. Hii ina maana kuwa katika uhakiki wa kimwingilianomatini hakuna mpaka baina ya fasihi na matini nyingine zisizo za kifasihi. Kwa hiyo ni ukweli kwamba, unapohakiki kazi kwa kutumia nadharia hii, unatakiwa kuhusisha matini nyingi. Kwa sababu, maana ya matini inakuwa ni kitu ambacho kinapatikana katika matini husika na matini nyingine zote zilizorejelewa na zinazohusiana nayo, yaani mwingilianomatini. Kwa mfano, riwaya ya *Marimba ya Majaliwa*, imeingiliana na matini za kijiografia, kihistoria na kisayansi kama tulivyoonesha katika sehemu iliyopita. Aidha, uhakiki wa kimwingilianomatini unahusisha mifumo ya kiutamaduni na desturi, hivyo, mhakiki anapaswa kuzingatia haya yote.

**5.0 Hitimisho**

Katika makala hii tumejaribu kufanya uhakiki wa kimwingilianomatini huku tukitoa mifano kutoka katika kazi za fasihi ya watoto na vijalunga. Kazi teule za fasihi ya watoto zilizoshughulikiwa katika Makala hii ni; *Sababu Mimi ni Mwanamke* (1999)

kilichoandikwa na Ebraju, *Ngome ya Mianzi* (2006) kilichoandikwa na Mulokozi, *Marimba ya Majaliwa* (2008), kilichoandikwa na Edwin Semzaba na *Kilio Chetu* (2008) kilichoandikwa na Medical Aid Foundation. Pia, tumejadili mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya uhakiki wa kimwingilianomatini kwenye kazi za kifasihi. Mambo ya msingi yaliyojadiliwa ni pamoja na suala la nadharia husika kuwa na mawanda mapana. Pia, tumeonesha jinsi kiwango cha maarifa aliyonayo mhakiki kuhusu matini chanzi kinavyoweza kuathiri ufanisi wa uhakiki wa kazi ya fasihi. Vilevile, tumezungumzia suala la nadharia tajwa kuwa na njia bainifu anuai ambazo ni muhimu kwa mhakiki kuzingatia. Aidha, suala la nadharia tajwa kuhusisha matini zisizo za kifasihi nalo limeonekana kuwa ni jambo la msingi la kuzingatia.

Kwa kumalizia, tunaweza kusema kwa hakika kuwa Nadharia ya Mwingilianomatini ni ya muhimu katika kuhakiki kazi za fasihi. Lengo la makala hii ni kuonesha madokezo na mambo ya muhimu kuhusu Nadharia ya Mwingilianomatini kwa wasomaji na wahakiki kazi za fasihi ili kuendelea kuisoma na kuitumia nadharia hii kwa upana na usahihi. Ni imani yetu kwamba mjadala tuliofanya katika makala hii utakuwa na mchango chanya katika utumiaji wa Nadharia ya Mwingilianomatini.

**Marejeleo**


Alfaro, M. J. M. (1996) “Intertextuality: Origions and Development of the Concept”. *Atlantis,* Juz. Na. 18(1), 268-285. http://www.jstor.org/stable/41054827 ilisomwa tarehe 10/11/2023.

Allen, G. (2000) *Intertextuality*. London: Routledge.

Bakize, L. H. (2014) *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bauman, R. (2004) *Cross-Cultural Perspectives on Intertextuality*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.

Clayton, J na Rothstein, E. (1991) *The Influence of Intertextuality in Literary History*. Wisconsin: The University of Wisconsin Press.

Ebraju, P. B. (1999) *Sababu Mimi ni Mwanamke*. Dar es Saalam: Educational Books Publishers.

Hebel, J. U. (1989) *Intertextuality: The Allusion and Quotation: an International Bibliography of Critical Studies*. California: Greenwood Press.

Himu, W. (2015) *Chanzo ni Wewe*. Dar es Salaam. Moccony Printing Press.

Irwin, W. (2004) “Against Intertextuality”. *Philosophy and Literature*, Juz. Na 28(2): 227-242. DOI:10.1353/phl.2004.0030 ilisomwa tarehe 12/11/23.

Ivanic, R. (1998) *Writing and Identity: The Discoursal Construction of Identity in Academic.* Amsterdam: John Benjamins Publishing Co.

Kahigi, K. K. (1995) “Lugha katika Vitabu vya Watoto”. *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 1:21-36.

Kristeva, J. (1980) *Desire in Language, A Semiotic Approach to Literature and Art.* New York: Colombia University Press.

Leitch, V. B. (1983) *Deconstructive Criticism*. New York: Colombia University Press.

Lyimo, E. B. (2014) “Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania”. *Mulika*, Juz. Na. 33:33-45.

Lyimo, E. B. (2018) *Dhima ya Mianzo na Miisho katika Nathari za Kiswahili na Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Riwaya na Hadithi za Watoto Nchini Tanzania*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mbatiah, W. (2001) *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi: Standard Textbook Graphics and Publishing.

Mbijima, R. J. (2020a) *Mkataa Pema na Ngano Nyingine*. Dar es Salaam: Seromercy Publishing Company Limited.

Mbijima, R. J. (2020b) *Udunu wangu: Ngonjera za Watoto*. Dar es Salaam: Seromercy Publishing Company Limited.

Medical Aid Foundation (2008) *Kilio Chetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (1989) “Tanzu za Fasihi Simulizi”. *Mulika*, Juzuu Na. 21: 2-11.

Mulokozi, M. M. (1990) *Ngoma ya Mianzi.* Dar es Salaam. TPH.

Mulokozi, M. M. (1996) *Moto ya Mianzi.* Dar es Salaam. ECOL Publications.

Mulokozi, M. M. (2014) *Ngome ya Mianzi*. Dar es Salaam. Kampuni ya Utamaduni: Tafsiri na Uchapishaji Tanzania.

Mulokozi, M. M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi Simulizi na Andishi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mnyanka, O. (2005) *Kimbia! Hellana! Kimbia!* Dar es Salaam. Heko Publisher Ltd.

Ndalu, A., Babusa, H na Mirikau, S (2014) *Kamusi Teule ya Kiswahili Kilele cha Lugha*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Ogede, O. (2011) *Intertextuality in Contemporary African Literature.* Maryland: Lexington Books.

Semzaba, E. (2008) *Marimba ya Majaliwa*. Dar es Salaam: E & D. Vission Publishing.

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wolfreys, J. (2004) *Critical Keyword in Literature and Cultural Theory*. London: Palgrave.